
policy forum




# UWAZI NA USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA UKUSANYAJI NA UGAWAJI WA USHURU WA HUDUMA UNAOTOKANA NA UCHIMBAJI MADINI. MIKOA YA GEITA NA MARA.

# UWAZI NA USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA UKUSANYAJI NA UGAWAJI WA USHURU WA HUDUMA UNAOTOKANA NA UCHIMBAJI MADINI. MIKOA YA GEITA NA MARA.

## 1. Utangulizi.

Sekta ya madini nchini Tanzania imepitia mageuzi makubwa ya kisheria na kisera tangu mwanzoni mwa mwaka 2000. Mabadiliko haya yalilenga zaidi kuhakikisha Tanzania kama nchi na hasa wananchi wake wanapata manufaa zaidi kutokana na maliasili waliyopewa na Mungu. Hata hivyo, manufaa hayo yanaweza kupatikana tu ikiwa utawala wa sekta ya madini kupitia ushiriki wa wananchi katika ukusanyaji na ugawaji wa mapato kutoka sekta hiyo utaboreshwa.

Nchini Tanzania, serikali ndio mmiliki halali wa madini yote (na maliasili nyingine) huku udhibiti wa maliasili hizo ukiwa chini ya Rais ambaye ndiye mdhamini pekee. Hii ina maana kwamba kuna wigo mdogo nchini wa kuruhusu kuweka sheria tofauti za kukusanya na kugawanya mapato ya madini kwa mamlaka za chini. Ili kuhakikisha mgawanyo sawa wa mapato ya madini kwa Watanzania wote, bajeti ya taifa hugawanya rasilimali zote za umma kwa kuzingatia vipaumbele vya serikali, ukubwa wa mapato yanayokusanywa na msongamano wa watu. Hivyo mamlaka za serikali za mitaa zina uwezo wa kuanzisha na kusimamia vyanzo mbalimbali vya mapato kama vile ushuru wa huduma na uwajibikaji wa Kampuni kwa jamii (CSR) ili kuwezesha maendeleo ya jamii. Kutokana na usuli huu, muhtasari huu unalenga kutoa matokeo ya uchambuzi wa ushiriki wa wananchi katika ukusanyaji na ugawaji wa ushuru wa huduma ya madini kwa kutumia Geita na Mara kama kisa mafunzo.

## 2. Matokeo ya Uchambuzi uliofanyika Geita na Mara.

Takwimu za msingi zilizotumika katika uchanganuzi zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 52 wanaoishi katika mikoa ya Geita na Mara. Wahojiwa 26 walihojiwa kwa kila mkoa. Wengi wa wahojiwa (asilimia 94.2) walikuwa na umri wa miaka 50 kuelekea chini, wakiakisi hali ya ujana ya watu wa Tanzania. Karibu asilimia 60 ya wahojiwa walikuwa wameoa au kuolewa. Idadi sawa ya wahojiwa wanawake na wanaume (50-50) walihojiwa ili kuakisi takwimu za kitaifa (51 dhidi ya 49 kwa idadi ya wanawake na wanaume).

Takwimu kwa ujumla hazikuonesha tofauti kubwa katika viwango vya elimu kimkoa. Hii inaonekana kuwa na athari katika kiwango cha uelewa wa ushuru wa huduma ya uchimbaji madini, ambayo mara nyingi haioneshi tofauti kubwa katika ngazi mbalimbali kwenye mikoa yote miwili.

Kiwango cha elimu kilichofikiwa na wahojiwa kilikuwa cha kuvutia sana kwani wote walikuwa wamesoma shule ya msingi au zaidi. Wakati robo yao walikuwa na sifa za shule ya sekondari, asilimia 67 walikuwa na sifa za elimu ya juu. Hii iliashiria kwamba wahojiwa wanaweza kufahamu maswali yaliyoulizwa na kutoa majibu sahihi.

Mwisho, ilidhaniwa kuwa kuishi kwenye eneo kwa muda mrefu, kungeathiri maarifa kuhusu mazingira kwa njia chanya. Kwa hiyo Kulikuwa na umuhimu wa kujua kutoka kwa waliohojiwa idadi ya miaka waliyoishi Geita au Mara. Ni 12 tu (asilimia 23) ambao wameishi kwenye maeneo hayo kwa miaka mitano au chini ya miaka hiyo na 21 kati

yao (asilimia 40) walikua wameishi kwenye maeneo ya migodi kwa zaidi ya miaka 15. Hii iliashiria kwamba waliohojiwa walikuwa na uelewa mzuri wa mazingira yao na walikuwa watu sahihi kwa ajili ya kuulizwa maswali.

Kwa kuwa majadiliano yanahusu ushuru wa huduma ya uchimbaji madini, ni muhimu kueleza jinsi inavyofikiwa. Kwa kifupi, Halmashauri hutoza asilimia 0.3 ya mapato ghafi ya madini ili kupata hisa zao za ushuru wa huduma. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa inayozipa mamlaka za serikali za mitaa kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango kisichozodo asilimia 0.3 ya mauzo ya kila mwaka ya makampuni ya madini.

Mchakato huo ni mgumu zaidi kwa wachimbaji wadogo (ASM) ambao hawauzi bidhaa zao katika vituo vya biashara ya madini kwani mbinu mbalimbali zinatumika kuhakikisha kwamba wanachangia pia sehemu yao ya ushuru wa huduma. Kwa mfano, kwa mujibu wa afisa mwandamizi wa serikali mkoani Geita, ASM wanatozwa TZS. 1,000 gunia lenye udongo wenye madini; TZS 21,000 kwa gari lenye uwezo wa chini ya tani 10 linalobeba udongo wenye madini TZS 30,000 kwa gari lenye uzito wa zaidi ya tani 10. Hivyo basi kwa vyovyote vile, wachimbaji wakubwa na wadogo huchangia sehemu yao ya ushuru wa huduma kutoka kwenye migodi ya madini.

## 2.1 Ushirikishwaji katika ukusanyaji na ugawaji wa mapato ya madini.

Kuna ushiriki mdogo wa jamii katika ukusanyaji na ugawaji wa ushuru. Kwa hakika, bila kujali umri, jinsia, kiwango cha elimu au idadi ya miaka wanaoishi katika maeneo ya migodi, idadi kubwa ya wahojiwa (34 kati ya 52) hawajui jinsi ushuru unavyokusanywa na kugawanywa katika maeneo ya migodi. Hali inaonekana kuwa mbaya zaidi mkoani Geita ambako wahojiwa 22 kati ya 26 wanasema hawajui ikilinganishwa na wahojiwa 12 wa Mara.

Haishangazi kwamba wahojiwa 10 tu mkoani Mara ndio wanafahamu ukweli kwamba baadhi ya mapato hugawanywa kwa makundi maalum kama vile wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wakati hakuna mtu mkoani Geita mwenye wazo la iwapo vikundi hivyo vinanufaika kutokana na ushuru wa huduma ya madini.

Lakini pia, wahojiwa 51 kati ya 52 hawakuwa na ufahamu kuhusu kiasi kilichokusanywa na Halmashauri katika mfumo wa ushuru wa huduma ya madini (angalia mfano Jedwali 1). Mbaya zaidi, idadi sawa ya wahojiwa waliripotiwa kutokuwa na taarifa kuhusu jinsi ushuru wa huduma unaokusanywa unagawanywa.

**Jedwali 1: Idadi ya wahojiwa (kwa umri) ambao wanajua kiasi cha ushuru wa huduma kilichokusanywa.**

| Je, unajua kiasi kinachokusanywa cha ushuru wa huduma? | | | Idadi ya miaka aliyoishi katika eneo | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Miaka 5-15 | Chini ya miaka 5 | Zaidi ya miaka 15 | |
| Ndio | Umri | 31-50 | | 1 | | **1** |
| | **Jumla** | | | **1** | | **1** |
| Hapana | Umri | 10-20 | 0 | 3 | 2 | **5** |
| | | 21-30 | 5 | 6 | 6 | **17** |
| | | 31-50 | 7 | 9 | 10 | **26** |
| | | Juu ya 50 | 0 | 0 | 3 | **3** |
| | **Jumla** | | **12** | **18** | **21** | **51** |
| **Jumla** | Umri | 10-20 | 0 | 3 | 2 | **5** |
| | | 21-30 | 5 | 6 | 6 | **17** |
| | | 31-50 | 7 | 10 | 10 | **27** |
| | | Juu ya 50 | 0 | 0 | 3 | **3** |
| | **Jumla** | | **12** | **19** | **21** | **52** |

Hata hivyo, inafurahisha kutambua tofauti za kimkoa katika suala la uelewa wa nani hasa anakusanya ushuru (Jedwali 2). Hususan, wakati wahojiwa kutoka Geita wana mwelekeo wa kuamini kuwa, ni serikali kuu (8) zaidi ya Halmashauri (5), ndiyo inayokusanya; wale wa Mara wanafikiri kuwa Halmashauri (13) ndizo zinazoweza kuwa wakusanyaji kuliko serikali kuu (2). Hii inaashiria haja ya kuongeza uelewa kwani jamii haziwezi kuiwajibisha serikali ikiwa hazijui mamlaka zinazosimamia ukusanyaji na ugawaji wa ushuru.

**Jedwali la 2: Nani hukusanya ushuru (kwa mkoa) ?**

| | | Nani anakusanya ushuru wa huduma? | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Serikali Kuu na Serikali za Mitaa | Serikali Kuu | Wananchi | Sijui | Mamlaka za Serikali za Mitaa | Hakuna jibu | |
| Mkoa | Geita | 1 | 8 | 0 | 2 | 5 | 10 | **26** |
| | Mara | 1 | 2 | 4 | 0 | 13 | 6 | **26** |
| **Jumla** | | **2** | **10** | **4** | **2** | **18** | **16** | **52** |

Hali hiyo inaweza kuwa mbaya zaidi kutokana na ukweli kwamba masuala yanayohusu ushuru wa huduma ya madini yanajadiliwa mara chache katika mikutano ya vijiji vya Mara na Geita. Kwa hakika, ni wahojiwa 2 tu kati ya 52 walioripoti kuwa walikuwa kwenye mkutano ambapo ukusanyaji na ugawaji wa ushuru wa huduma ulikuwa mada ya majadiliano. Hii ina maana kwamba jamii ni mara chache sana kushirikishwa, katika mchakato wa kukusanya na kugawanya ushuru wa huduma.

Kinachoonekana wazi ni ukweli kwamba jamii zinataka kuhusishwa. Kwa hakika, wahojiwa 45 kati ya 52 wanafikiri jamii za maeneo husika zinahitaji kuhusishwa katika kukusanya na kugawanya ushuru. Wanaume 4 na wanawake 2 pekee walipinga hitaji la kuhusika kwa jamii ikipelekea kutokuwepo kwa tofauti kubwa ya kitakwimu ya kijinsia katika jibu hili mahususi. Vile vile, matokeo hayaoneshi tofauti kubwa za kitakwimu katika majibu katika umri, kiwango cha elimu, hali ya ndoa na miaka ya kuishi katika maeneo yanayozunguka migodi.

## 2.2 Kiwango ambacho vikundi mbalimbali vya kijamii vinanufaika na ushuru wa huduma.

Ushuru wa huduma unatarajiwa kunufaisha jamii kwa ujumla iwapo utasimamiwa vyema kwakuwa unaunda chanzo muhimu cha mapato katika maeneo ya madini. Kwa mfano, kwa mujibu wa afisa mmoja mwandamizi wa serikali mkoani Mara, "ushuru wa huduma ya madini ni asilimia 75 ya mapato yote ya ndani katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime". Haikushangaza basi kwamba huko Geita na Mara, wahojiwa 38 (asilimia 73) walidai kufahamu faida zinazohusishwa na ushuru wa madini (Jedwali 3).

**Jedwali la 3: Idadi ya wahojiwa (katika jinsia na miaka walioishi katika eneo) ambao wanadai kujua faida zinazotokana na ushuru wa huduma.**

| **Je, unajua manufaa yoyote yanayotokana na ushuru wa huduma katika jumuiya yako?** | | | **Uzoefu** | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Chini ya miaka 5 | Miaka 5-15 | Zaidi ya miaka 15 | |
| Ndio | Jinsia | Mwanaume | 2 | 6 | 11 | **19** |
| | | Mwanamke | 4 | 7 | 8 | **19** |
| | **Jumla** | | **6** | **13** | **19** | **38** |
| Hapana | Jinsia | Mwanaume | 2 | 4 | 1 | **7** |
| | | Mwanamke | 4 | 2 | 1 | **7** |
| | **Jumla** | | **6** | **6** | **2** | **14** |
| **Jumla** | Jinsia | Mwanaume | 4 | 10 | 12 | **26** |
| | | Mwanamke | 8 | 9 | 9 | **26** |
| | **Jumla** | | **12** | **19** | **21** | **52** |

Idadi kubwa ya wahojiwa (32 kati ya 52) waliorodhesha utoaji na uboreshaji wa huduma za jamii kama vile barabara, shule, hospitali na maji kama aina ya manufaa ambayo hufaidika zaidi kupitia marejesho ya ushuru wa huduma ya uchimbaji madini (angalia kielelezo 1). Takwimu zinaonesha hakuna mgawanyo muhimu wa kijinsia kitakwimu katika majibu kati ya wahojiwa hawa (wahojiwa 19 wa kiume na wa kike) na mgawanyo wa hali ya ndoa (20 kwa wenye ndoa na 18 waliohojiwa ambao hawana ndoa).

**Kielelezo 1: Miundombinu ya shule huko Geita & Mara iliyojengwa kupitia mapato ya ushuru wa huduma.**






Hata hivyo, Jedwali la 3 linaonesha kuwa watu waliokuwa wakiishi karibu na eneo la migodi kwa muda mrefu walikuwa na uwezekano mkubwa wa kujua manufaa. Hakika, kati ya wahojiwa 38 ambao wanajua faida za ushuru, 32 kati yao walikuwa wameishi katika eneo hilo kwa miaka mitano au zaidi. Hii inaashiria kwamba kadiri watu walivyoishi kwa muda mrefu katika mazingira ya uchimbaji madini, ndivyo walivyoweza kupata uelewa wa manufaa ya ushuru wa huduma. Aidha, wahojiwa 36 kati ya 38 waliodai kufahamu manufaa ya ushuru wana viwango vya elimu ya sekondari (11) au elimu ya juu (25). Hii ina maana kwamba wanajamii walioelimika wako katika nafasi nzuri zaidi ya kuthamini manufaa yanayoletwa na ushuru wa huduma.

Wasiwasi mmoja kutoka kwa wengi wa wahojiwa (48 kati ya 52) ni kwamba faida zinazotokana na ushuru wa huduma hazigawanywi sawasawa kwa vikundi tofauti vya kijamii (Jedwali 4). Idadi hiyo inajumuisha wahojiwa walioelimika (44) na watu ambao wameishi karibu na maeneo ya migodi kwa muda mrefu (32). Kwa kuwa vigezo vyote viwili, elimu na idadi ya miaka aliyoishi karibu na maeneo ya uchimbaji madini ni muhimu katika kupima uwezo wa mtu binafsi kufahamu mazingira, hakuna shaka kwamba mgawanyo wa ushuru wa huduma kwa makundi mbalimbali ya kijamii unahitaji kuboreshwa.

**Jedwali la 4: Idadi ya wahojiwa (kwa hali ya ndoa na viwango vya elimu) ambao wanafikiri faida kutoka kwenye ushuru wa huduma zinagawanywa kwa usawa kwa vikundi tofauti vya kijamii.**

<table>
<tr><th colspan="3" rowspan="2">Je, manufaa kutoka kwenye ushuru yanasambazwa kwa usawa katika makundi mbalimbali ya kijamii?</th><th colspan="3">Kiwango cha elimu</th><th rowspan="2">Jumla</th></tr>
<tr><th>Elimu ya msingi</th><th>Elimu ya sekondari</th><th>Elimu ya juu</th></tr>
<tr><td rowspan="2">Ndio</td><td>Hali ya ndoa</td><td>Hajaoa / hajaolewa</td><td></td><td>1</td><td>3</td><td>4</td></tr>
<tr><td colspan="2">Jumla</td><td></td><td>1</td><td>3</td><td>4</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Hapana</td><td rowspan="2">Hali ya ndoa</td><td>Ameoa / Ameolewa</td><td>2</td><td>3</td><td>20</td><td>25</td></tr>
<tr><td>Hajaoa / hajaolewa</td><td>2</td><td>6</td><td>9</td><td>17</td></tr>
<tr><td colspan="2">Jumla</td><td>4</td><td>9</td><td>29</td><td>42</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Sijui</td><td rowspan="2">Hali ya ndoa</td><td>Ameoa / Ameolewa</td><td></td><td>2</td><td>0</td><td>2</td></tr>
<tr><td>Hajaoa/hajaolewa</td><td></td><td>1</td><td>3</td><td>4</td></tr>
<tr><td colspan="2">Jumla</td><td></td><td>3</td><td>3</td><td>6</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Jumla</td><td rowspan="2">Hali ya ndoa</td><td>Ameoa / Ameolewa</td><td>2</td><td>5</td><td>20</td><td>27</td></tr>
<tr><td>Hajaoa / hajaolewa</td><td>2</td><td>8</td><td>15</td><td>25</td></tr>
<tr><td colspan="2">Jumla</td><td>4</td><td>13</td><td>35</td><td>52</td></tr>
</table>

## 2.3 Uelewa wa jamii kuhusu ukusanyaji na ugawaji wa ushuru wa huduma.

Ujuzi wa kusoma na kuandika ni muhimu katika kuzifanya jamii kuwa na hamu na ikiwezekana kujihusisha katika ukusanyaji na ugawaji wa ushuru. Ilikuwa vizuri kuona kwamba idadi kubwa ya wahojiwa (38 kati ya 52) walidai kufahamu kuwepo kwa ushuru wa huduma unaotokana na uchimbaji madini. Ingawa inaonekana kuwa ya kuvutia, kiwango hiki cha uelewa hakina maana kubwa kwani wahojiwa wengi (51 kati ya 52) waliripoti kutokuwa na ufahamu kuhusu kiasi halisi kilichokusanywa kama ushuru katika mikoa ya Geita na Mara. Kipimo cha kijinsia hakikuonesha tofauti yoyote ya kitakwimu miongoni mwa wahojiwa wanaodai kufahamu kuhusu ushuru wa huduma (wanaume 20 na wahojiwa 18 wa kike).

Kukosekana kwa ufahamu wa kiasi kilichokusanywa kunaweza kuwa ni matokeo ya tabia ya halmashauri kuchanganya mapato yake yote kwenye kapu moja. Kwa hakika, kwa mujibu wa afisa mwandamizi wa serikali mkoani Mara, "mapato yatokanayo na ushuru wa huduma kwa kawaida huongezwa kwenye mapato mengine ya ndani tayari kutumika katika kutekeleza miradi mbalimbali ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime". Kwa hakika hii inafanya ukaguzi wa ushuru wa huduma kuwa mgumu sana. Kuna haja ya kuhakikisha kwamba mapato yanayotokana na ushuru wa huduma yanatenganishwa na mapato mengine ya ndani ili kuruhusu ukaguzi wa kina wa matumizi yake.

Ni muhimu kutambua kwamba wengi wa wahojiwa waliodai kufahamu masuala ya ushuru wameelimika (Jedwali 5). Kwa hakika, wahojiwa 26 kati ya 38 waliodai kufahamu ushuru wa huduma walikuwa na elimu ya juu, 9 kati yao walikuwa na elimu ya sekondari na wa 3 tu walikuwa na sifa za elimu ya msingi.

Hii ina maana kwamba elimu ni kigezo muhimu linapokuja suala la wananchi kudai ushirikishwaji zaidi katika kusimamia rasilimali za umma.

**Jedwali la 5: Idadi ya wahojiwa (kwa ngazi ya jinsia na elimu) wanaodai kufahamu kuhusu ushuru wa huduma kutoka kwenye migodi ya madini.**

| Je, unafahamu kuhusu ushuru wa huduma? | | | Kiwango cha elimu | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Elimu ya Msingi | Elimu ya sekondari | Elimu ya juu | |
| Ndio | Jinsia | Mwanaume | 2 | 3 | 15 | **20** |
| | | Mwanamke | 1 | 6 | 11 | **18** |
| | **Jumla** | | **3** | **9** | **26** | **38** |
| Hapana | Jinsia | Mwanaume | 0 | 2 | 4 | **6** |
| | | Mwanamke | 1 | 2 | 5 | **8** |
| | **Jumla** | | **1** | **4** | **9** | **14** |
| Jumla | Jinsia | Mwanaume | 2 | 5 | 19 | **26** |
| | | Mwanamke | 2 | 8 | 16 | **26** |
| | **Jumla** | | **4** | **13** | **35** | **52** |

Idadi ya miaka ya kuishi karibu na maeneo ya uchimbaji madini pia inaonekana kuwa muhimu linapokuja suala la ufahamu wa ushuru unaotokana na uchimbaji madini. Kwa hakika, wahojiwa 31 kati ya 38 waliodai kufahamu kuhusu ushuru waliishi katika maeneo hayo kwa miaka mitano au zaidi. Nafasi za uongozi katika kamati zinazohusiana na ukusanyaji na ugawaji wa ushuru wa huduma lazima zizingatie muda ambao mtu ametumia maisha yake katika maeneo yanayozunguka uchimbaji madini.

## 2.4 Mapendekezo ya jinsi ya kuboresha hali kutoka kwa waliohojiwa

Kila mhojiwa alitakiwa kutaja jambo moja linalopaswa kufanywa ili kuboresha mchakato wa kukusanya na kugawanya ushuru wa huduma mkoani Geita na Mara. kwa ujumla walitoa mapendekezo yanayojadiliwa kwa ufupi hapa chini:

i. Uboreshaji na utekelezaji wa mipango, sera na mifumo ya kisheria. Wahojiwa wanaamini kuwa mfumo sahihi wa udhibiti utahakikisha kuwa kila kitu kinatekelezwa kwa njia ambayo ni ya manufaa kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya uchimbaji madini. Serikali inapaswa kuzingatia na kutekeleza sheria na hasa bunge litoe maamuzi kuhusu masharti ya mikataba ya madini ambayo hayana mashiko.

ii. Uboreshaji wa upatikanaji wa elimu pia umetajwa kuwa jambo muhimu katika kuhakikisha ukusanyaji na ugawaji wa manufaa ya ushuru wa huduma. Elimu ni muhimu kwani inakuza uwezo wa jamii kufahamu mazingira yao na hivyo kuiwezesha kusimamia ipasavyo ukusanyaji na ugawaji wa ushuru wa huduma. Ni muhimu kutambua kwamba wakati wahojiwa wengi mkoani Mara (20) kuliko Geita (10) walipendekeza elimu kama suluhu, wahojiwa wengi zaidi mkoani Geita (8) kuliko Mara (3) walidhani kuwa uhamasishaji kuhusu ushuru wa huduma katika jamii ungetosha.

Ujumbe muhimu hapa ni kwamba, Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanapaswa kutoa kiwango fulani cha uelewa kwa jamii ili ziweze kuwa na ushawishi chanya katika ukusanyaji na ugawaji wa ushuru wa huduma unaotokana na uchimbaji madini.

iii. Serikali ina haja ya kuboresha utawala bora kuhusu ukusanyaji na ugawaji wa ushuru wa huduma. Hili linapaswa kuhusisha kuimarishwa kwa uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini. Kwa upande mwingine, hatua hiyo ingepelekea kuboreshwa kwa ukusanyaji na ugawaji wa ushuru kuzunguka maeneo ya uchimbaji madini. Hili linaweza kufanyika kwa kuhakikisha kuwa ripoti za TEITI zinatolewa na zinapatikana hadharani kama sheria inavyotaka na mikataba iliyosainiwa katika sekta ya madini inatolewa wazi kwa umma.

iv. Ushiriki wa jamii na ushirikishwaji pia ulitolewa kama njia ya kusonga mbele. Wahojiwa waliamini kuwa, ushirikishwaji huo ungehakikisha usimamizi mzuri wa ushuru kwani ushiriki wao ungechochea utawala bora na mgawanyo sawa wa faida kutoka kwenye ushuru unaokusanywa. Takribani wahojiwa 6 kutoka Mara walitaka jamii zishirikishwe katika ngazi zote za ukusanyaji, upangaji na ugawaji wa fedha kutoka kwenye ushuru, hakuna aliyefikiria hivyo huko Geita. Hii inaonesha kuwa jamii za Mara zinaweza kuwa makini zaidi kuliko Geita. Serikali inahitaji kushirikisha jamii kikamilifu katika kukusanya na kugawanya ushuru wa huduma ya uchimbaji madini. Ushiriki wa wananchi lazima ufanyike katika ngazi mbili: (i) Ngazi ya jamii: wananchi wa kawaida lazima wawe sehemu ya kamati zinazosimamia ukusanyaji na ugawaji wa ushuru na kuwa sehemu ya ajenda ya kudumu ya mikutano yote ya kijiji. (ii) Ngazi ya serikali: bunge na mabaraza yanapaswa kutekeleza wajibu wao wa uwakilishi kwa kuzingatia zaidi maslahi ya wapiga kura. Hili litaimarisha utawala bora na hatimaye kuboresha matokeo ya sera.

v. Serikali kuimarisha usalama na haki za binadamu kama suluhisho ambalo linaweza kuleta ukusanyaji na ugawaji sahihi wa ushuru wa huduma. Hii inaweza kuashiria kwamba kujiingiza katika biashara ya kukusanya na kugawanya ushuru wa huduma za uchimbaji madini kunaweza kuwa si jambo salama sana. Inapendekezwa kuwa ombi hili lifanyiwe uchunguzi wa kina zaidi.

vi. Serikali ihakikishe kuwa faida zinazopatikana kutokana na ushuru wa huduma ya uchimbaji madini zinasambazwa kwa namna ambayo itaongeza manufaa sawa kwa makundi mbalimbali ya kijamii wakiwemo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kujenga miundombinu kwa ajili ya utoaji wa huduma za kijamii kunaweza kutokidhi mahitaji ya makundi yote ya kijamii. Hili linaweza kuimarishwa kwa kufanya tathmini ya mahitaji katika jamii ili kubaini mahitaji shindani na baadaye kuja na vipaumbele vinavyohusu jamii nzima na kupitia upya vipaumbele vya jamii mara kwa mara ili kuakisi mabadiliko ya demografia na mahitaji katika maeneo ya uchimbaji madini kupitia majadiliano ya mara kwa mara kuhusu ushuru wa huduma ya uchimbaji madini katika mikutano ya kijiji, halmashauri na bunge.

***Chanzo:*** *Utafiti wa Uwazi na Ushiriki wa Wananchi katika Ukusanyaji na Ugawaji wa Ushuru wa Huduma ya Madini, Mikoa ya Geita na Mara.*

policy forum


Ndovu Street (Tancom Street), off Rose Garden Road

P.O. Box 38486, Dar es Salaam

Tel: +255 22 2780200

Mobile: +255 782 317 432

Email: info@policyforum.or.tz

Website: www.policyforum.or.tz